# Msofe ataka wawekezaji waanze kulipa kodi

Na Mwandishi Wetu.

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Ilala, Mohammed Msofe, amecharuka, baada ya kuwataka wawekezaji wa flemu za maduka kuanza kulipa kodi ili pande zote mbili ziweze kunufaika na mapato.

Msofe aliyasema hayo Agosti 15, mwaka huu, wakati akizungumza na wawekezaji katika Kata ya Zingiziwa, Ilala, jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti huyo ambaye aliambatana na Kamati ya Utekezaji Wazazi CCM Wilaya ya Ilala, alisema kuwa kitendo cha wawekezaji hao kuendelea kukaa bure bila kulipa kodi ni kuinyima jumuiya hiyo mapato.

"Nataka wawekezaji wanaofanya biashara katika eneo hili, kufika ofisini ili tuweze kuweka utaratibu wa kukubaliana namna ya kulipa kodi," alisema Msofe.

Msofe alisema haiwezekani wawekezaji hao waendelee kukaa bure katika flemu hizo bila kulipa kodi, kwani wanarudisha nyuma maendeleo ya jumuiya ya wazazi CCM.

Wawekezaji hao ambao wana muda wa zaidi ya miaka tisa kuanzia mwaka 2018, Msofe alisema kuwa ifike wakati sasa waanze kulipa kodi bila kujali mwenye flemu ameanza kufanya biashara au la.

Mwenyekiti huyo alisema anataka kuona kila mwekezaji ambaye atafanyabiashara katika eneo lao lililopo Zingiziwa anazingatia utaratibu wa kulipa kodi.

"Haiwezekani upande mmoja unufaike wakati mwingine haupati mapato yoyote, tunarudisha nyuma jumuiya," alisema.

Kamati hiyo ya Utekelezaji chini ya Msofe ilipata nafasi ya kuongea na wawekezaji kwa lengo la kujua changamoto zinazokwamisha uendelezaji wa ujenzi wa flemu za maduka katika eneo hilo.

Baadhi ya wawekezaji hao walisema kuwa changamoto zilizokuwapo ni pamoja na mgogoro wa ardhi katika eneo hilo.

Mmoja wa wawekezaji hao, Manufred Ndunguru alisema kuwa sababu hiyo iliwafanya washindwe kuendelea na uwekezaji.

Akijibu hoja za wawekezaji hao, Msofe alisema kuwa eneo hilo kwa sasa ni salama na halina mgogoro wowote.

# DCEA yateketeza ekari 603 mashamba ya bangi

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imeteketeza ekari 603 za mashamba ya bangi na kukamata magunia 49 ya bangi katika operesheni maalum iliyofanyika Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro, huku watuhumiwa 13 wakikamatwa kuhusisiana na mashamba hayo.

Operesheni hiyo ilifanyika mwiahoni mwa wiki, katika vijiji vya Misengele, Lugenge, Kisaki na Nyarutanga, pia ilibaini na kuharibu kambi 21 zilizokuwa zikitumiwa na wakulima wa bangi.

Akizungumza kuhusu operesheni hiyo, Kamishna Jenerali wa DCEA Aretas Lyimo, alisema hatua hiyo ni sehemu ya mkakati endelevu wa Serikali wa kudhibiti uzalishaji wa dawa za kulevya nchini, hususan bangi, ambayo imeendelea kuzalishwa katika baadhi ya maeneo ya nchi.

Alisema, operesheni hizo zimebaini mabadiliko katika mbinu zinazotumiwa na baadhi ya wakulima wa bangi, ambapo wanahamisha shughuli zao kutoka maeneo yaliyofikiwa na operesheni na kuingia ndani zaidi ya maeneo ya hifadhi.

"Tumebaini kuwa baadhi ya wakulima wamehamishia shughuli zao ndani zaidi ya maeneo ya hifadhi ili kukwepa hatua za kisheria. Hali hii inachangia uharibifu mkubwa wa mazingira kupitia ukataji wa miti ovyo, uvamizi wa vyanzo vya maji na kuathiri mfumo wa ikolojia," alisema Lyimo.

Kwa mujibu wa Lyimo, tathmini ya operesheni zilizotekelezwa na DCEA tangu mwaka 2023 imeonyesha kuwa, licha ya mashamba mengi ya bangi kubainika na kuteketezwa katika Mkoa wa Morogoro, baadhi ya wahusika wameendelea kubadilisha maeneo ya uzalishaji na kujificha ndani ya maeneo ya hifadhi.

Alisema, hali hiyo inahitaji ushirikiano wa karibu zaidi kati ya DCEA, vyombo vya ulinzi na usalama, mamlaka zinazosimamia maeneo ya hifadhi na wananchi ili kuzuia maeneo hayo kutumiwa kwa uzalishaji wa dawa za kulevya.

Lyimo aliwataka wasimamizi wa maeneo ya hifadhi kuhakikisha maeneo wanayoyasimamia hayatumiki kwa kilimo cha bangi, huku akisisitiza kuwa mapambano dhidi ya uzalishaji wa dawa za kulevya yanahitaji ushirikiano wa taasisi na jamii.

DCE itaendelea kufanya operesheni jumuishi katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, mamlaka za uhifadhi na wananchi ili kudhibiti kilimo na biashara haramu ya bangi.

Sambamba operesheni hizo, Lyimo alisema Mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya dawa za kulevya na kuhamasisha wananchi kutoa taarifa kuhusu watu wanaojihusisha na uzalishaji, usafirishaji na biashara haramu ya dawa za kulevya.




Meneja Mauzo wa Shirika la Posta Tanzania Philip Koweri(kulia), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika ofisi za Posta mkoani Mwanza,namna ambavyo shirika hilo limeboresha huduma ya EMS katika utoaji huduma kidigitali huku kushoto ni Meneja wa huduma ya EMS wa Shirika la Posta Tanzania Ahmad Rashid. (Picha na Judith Ferdinand)

# Vijana wapatiwa mafunzo kidijitali Zanzibar

Na Mwandishi Wetu

ZAIDI ya vijana na wanawake 300 Zanzibar wamepatiwa mafunzo ya ujuzi wa kidijitali na ujumuishaji wa kifedha kupitia mpango wa Airtel Fursa Lab, huku Airtel Tanzania ikilenga kuwasaidia wananchi kutumia teknolojia kama nyenzo ya kujenga fursa za kiuchumi.

Mafunzo hayo yaliyotekelezwa kwa ushirikiano na Dar Teknohama Business Incubator (DTBi) wakati wa Tamasha la Kizimkazi 2026, yalihusisha masomo ya programu za kompyuta, matumizi ya kompyuta, akili bandia (AI), roboti, uundaji wa programu, ubunifu na ujasiriamali.

Mpango huo unaendana na ongezeko la matumizi ya intaneti na huduma za fedha kwa njia ya simu nchini Tanzania, ambapo upatikanaji wa teknolojia unaendelea kufungua fursa mpya za kiuchumi. Hata hivyo, ukosefu wa ujuzi wa kiteknolojia na biashara unaweza kuwazuia watumiaji kunufaika kikamilifu na fursa hizo.

Katika Skuli ya Sekondari ya Biashara Zanzibar, wanafunzi walipata fursa ya kujifunza matumizi ya teknolojia kwa vitendo, ikiwemo programu za kompyuta na uundaji wa michoro hai (animation).

"Teknolojia inaweza kufungua fursa kwa vijana na kuwasaidia kubadili maisha yao," alisema Grace Mgaya kutoka Airtel Tanzania baada ya mafunzo yaliyofanyika shuleni hapo.

Alisema, Airtel Fursa Lab inashirikiana na wadau, wakiwemo DTBi, kuwasaidia vijana kutumia teknolojia kuanzisha biashara, kubuni bidhaa na huduma pamoja na kutafuta fursa za kiuchumi.

Elia Kinshaga, Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa DTBi, alisema ushirikiano kati ya Airtel Tanzania, Airtel Africa Foundation na DTBi unalenga kujenga ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano kwa wanafunzi, huku ukiwapatia wanawake na vijana wanaojishughulisha na minyororo ya thamani au kujiajiri maarifa ya ujumuishaji wa kifedha.

Mchanganyiko wa ujuzi wa kiteknolojia na kifedha unalenga kushughulikia changamoto mbili za ushiriki katika uchumi wa kidijitali, uwezo wa kutumia teknolojia na uwezo wa kuitumia kuzalisha kipato.

Naye Yasir Hassan, mwanafunzi wa Kidato cha Tano katika Skuli ya Sekondari ya Biashara Zanzibar, alisema wanafunzi walitambulishwa katika misingi ya programu za kompyuta kupitia zana kama Scratch 3, inayowawezesha kutengeneza michoro hai na miradi shirikishi.

Salha Abdallah, mwanafunzi wa Kidato cha Tatu katika skuli hiyo, alisema wanafunzi pia walijifunza namna ya kutengeneza michezo ya kompyuta na miradi mingine kwa kutumia teknolojia.

Alisema ujuzi huo unaweza kuwasaidia wanafunzi kujiajiri katika siku zijazo.Skuli ya Sekondari ya Biashara Zanzibar ilikaribisha mpango huo kama nyongeza muhimu katika elimu rasmi, hasa kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya kompyuta na biashara.

Airtel Tanzania ilisema mafunzo ya Airtel Fursa Lab ni sehemu ya juhudi zake pana kupitia Airtel Kila Kona, zinazolenga kuunga mkono mabadiliko ya kidijitali na maendeleo ya jamii.

Kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, ambako idadi kubwa ya vijana inaingia katika soko la ajira, upatikanaji wa ujuzi wa vitendo wa kidijitali unazidi kuwa muhimu huku biashara na huduma zikihamia zaidi katika mifumo inayotegemea teknolojia.